

**Kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei ya mwaka 2007 katika kipindi cha 2007 - 2013**




***Mchango wa Pato la Taifa kwa aina ya Matumizi*** 2013




## 5. Matumizi ya Pato la Taifa

- Kupima jinsi uchumi wa nchi unavyoongezeka baada ya muda;
- Kiashiria cha Uchumi ambacho hutumiwa na nchi katika kupanga na ufuatiliaji mipango ya kijamii na kiuchumi

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**

*Dira*

*"Kuwa chanzo cha kuaminika katika kutoa takwimu rasmi nchini Tanzania"*


*Dhamira*

*"Kutoa takwimu rasmi na huduma za kitakwimu zina-zokidhi mahitaji ya watumiaji wa takwimu wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kupanga mipango na kufanya maamuzi sahihi."*


**Kwa mawasiliano zaidi**
**Wasiliana na:** Mkurugenzi Mkuu
Ofisi ys Taifa ya Takwimu
18 Barabara ya Kivukoni
S.L.P. 796
11992 - Dar es Salaam
Tanzania
Simu: (+255) 22 2122722/3
Nukushi: (+255) 22 2130852
Barua pepe: dg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA ZILIZOREKEBISHWA KWA TANZANIA BARA KWA BEI ZA MWAKA, 2007





**OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU**
**WIZARA YA FEDHA**

**Dar Es Salaam**
**Desemba, 2014**

## 1. Kwa nini kurekebisha Takwimu za Pato la Taifa Tanzania Bara?

Marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa Tanzania Bara yamekuwa yakifanyika kwa sababu zifuatazo:

(i) Mwaka wa kizio wa 2001 umepitwa na wakati na wala hauakisi mabadiliko ya kimuundo ambayo yamejitokeza katika uchumi;

(ii) Kujumuisha mabadiliko ambayo yamefanyika hasa katika mifumo ya uzalishaji, matumizi na uwekezaji katika uchumi;

(iii) Kujumuisha bidhaa katika uchumi, kama maendeleo endelevu na ubunifu unavyosababisha bidhaa mpya kuonekana katika soko wakati bidhaa zilizopitwa na wakati hutoweka katika soko;


(iv) Kuingiza taarifa mpya zilizopatikana kutoka katika tafiti za kaya kulingana na tafiti za msingi; na

(v) Kujumuisha matakwa mapya ya mfumo wa kimataifa wa takwimu za uchumi kwa mujibu wa chapisho la 1993 na 2008, na kuzingatia mabadiliko ya miongozo ipasavyo.

## 2. Kiwango cha Mabadiliko kati ya Patola Taifa kabla na baada ya marekebisho

Uchambuzi wa takwimu za Pato la Taifa umejengwa katika msingi wa ulinganifu kati ya takwimu za mwaka wa kizio wa 2001 na zilizorekebishwa kwa mwaka wa kizio wa 2007. Thamani ya Pato la Taifa lililorekebishwa kwa mwaka 2007 ni TSh. Milioni 26,770,432 ikilinganishwa na TSh. 20,948,403, za Pato la Taifa la mwaka 2007 kabla ya marekebisho, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 27.8.

Matokeo yanaonyesha kwamba, mabadiliko ya juu ni





katika huduma nyingine za kijamii na binafsi kwa badiliko la asilimia 232.1, wakati umeme na gesi umekuwa chini kwa badiliko la asilimia -30.7, Jedwali 1.

**Jedwali 1: Pato la Taifa kwa Mwaka 2007 katika Bei ya sasa kwa 2001 na 2007**

| Shughuli za Kiuchumi | 2001 | 2007 | Badiliko la Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mazao, uwindaji na misitu | 5,413,257 | 6,756,585 | 24.8 |
| Uvuvi | 277,189 | 424,772 | 53.2 |
| Madini na Uchimbaji Mawe | 742,932 | 935,412 | 25.9 |
| Viwanda | 1,625,504 | 1,908,283 | 17.4 |
| Umeme na Gesi | 335,898 | 232,622 | -30.7 |
| Maji | 84,982 | 208,528 | 145.4 |
| Ujenzi | 1,641,741 | 2,117,074 | 29 |
| Biashara na Matengenezo | 2,416,506 | 2,740,461 | 13.4 |
| Hoteli na Migahawa | 559,722 | 481,997 | -13.9 |
| Uchukuzi | 886,844 | 1,600,183 | 80.4 |
| Mawasiliano | 487,132 | 481,416 | -1.2 |
| Fedha | 345,000 | 756,075 | 119.2 |
| Upangishaji Majengo na Huduma za Biashara | 1,982,107 | 2,737,640 | 38.1 |
| Utawala | 1,652,556 | 2,249,818 | 36.1 |
| Elimu | 289,617 | 851,208 | 193.9 |
| Afya | 327,658 | 438,415 | 33.8 |
| Huduma nyingine za Kijamii na Binafsi | 129,482 | 430,055 | 232.1 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani kabla ya Marekebisho** | **19,198,125** | **25,350,544** | **32.0** |
| *Toa Ushuru wa Huduma za Mabenki* | -208,281 | -401,656 | 92.8 |
| *Ongeza Kodi katika Bidhaa* | 1,958,559 | 1,821,544 | -7.0 |
| **Jumla ya Pato la Taifa** | **20,948,403** | **26,770,432** | **27.8** |

## 3. Mchango wa Pato laTaifa kwa Shughuli kuu za Kiuchumi kwa bei ya sasa mwaka 2013

Jumla ya Thamani ya Pato la Taifa kwa mwaka 2013 (bei ya miaka inayohusika) ilikuwa Tsh. 69.8 trilioni wakati wastani wa Pato kwa kila Mtu ni Tshs. 1,561,050.




Shughuli za kiuchumi za Huduma zina mgao mkubwa zaidi wa Pato la Taifa wa asilimia 43.7 wakati Viwanda na Ujenzi vina mgao wa takribani ya asilimia 22.7.

## 4.Kiwango Halisi cha Ukuaji

Viwango vya ukuaji halisi ni kipimo kwa asilimia ya mabadiliko ya Pato la Taifa kwa mwaka husika ikilinganishwa na Pato la Taifa kwa mwaka uliotangulia.

Ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka 2013 uliongezeka kwa asilimia 7.3 kutoka asilimia 5.1 mwaka 2012. Viwango vya ukuaji wa mwaka 2013 kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi vinaonyesha kuwa Kilimo, misitu na uvuvi zilikua kwa asilimia 3.2; shughuli za viwanda zilikua kwa asilimia 6.6; na shughuli za Biashara zilikua kwa asilimia 5.3